



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO



Unapojibu tafadhali taja;

Kumb. Na. EA.101/165/01B/239

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
Mtaa wa Shaaban Robert,
S.L.P. 938,
DODOMA.




06 Julai, 2023

Kuh: KUTOA ELIMU YA MATUMIZI YA TEHAMA SERIKALINI

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019 yenye jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma.
3. Katika utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao, e-GA imekuwa ikiendesha programu maalumu ya kutoa elimu kwa Taasisi za Umma juu ya Huduma mbalimbali zinazotolewa na Mamlaka pamoja na Utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao ili kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA katika Taasisi za Umma yanazingatiwa ipasavyo.
4. Kwa barua hii, Mamlaka inaomba nafasi ya kukutana na Menejimenti ya Taasisi yako kwa tarehe mtakayopendekeza kati ya mwezi Julai hadi Septemba, 2023 kwa ajili ya kutoa elimu ya matumizi ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa shughuli za Serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi.
5. Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na Bi. Queenter Mawinda kwa simu namba **0657775780** au barua pepe queenter.mawinda@ega.go.tz.

Ninakushukuru kwa ushirikiano wako.


Eng. Benedic UB. Ndomba
MKURUGENZI MKUU